Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.36 - 2024

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*




## Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023

## Sasa Rasmi

# Rais Samia aweka jiwe la msingi Chuo cha VETA Rukwa



## - KAZI IENDELEE -




## BODI YA UHARIRI

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
***Kamishna wa Elimu***

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## Shahada za Amali kuchochea maendeleo kiuchumi

Serikali ya Tanzania inatambua haki ya kila mtu kupata elimu, kutimiza jukumu hilo muhimu kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaendelea kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu, kwa kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuboresha miundombinu ya ujifunzaji kuhakikisha upatikanaji wa viwango bora vya elimu na mafunzo katika ngazi zote, ili kuwawezesha Watanzania kupata stadi stahiki na umahiri.

Hivi karibuni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alifanya ziara ya kikazi Mkoani Rukwa, ambapo alipata nafasi kujionea maendeleo ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo katika sekta ya elimu, hii ni pamoja na kuzindua mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga, kuweka jiwe la msingi la Chuo Cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Rukwa na kuweka jiwe la msingi ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Sayansi iliyopo iliyopo Kijiji cha Mtindilo Laela katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

Katika ziara hiyo Julai 17, 2024 Watanzania tumeshuhudia Mhe. Rais akiweka jiwe la Msingi Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya Kampasi ya Rukwa, inayotarajiwa kutoa shahada za Amali ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mageuzi ya elimu nchini yanayolenga kuongeza hamasa ya kukuza elimu, ujuzi na matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kusaidia Taifa kutatua changamoto mbalimbali na kuchagiza maendeleo kiuchumi.

MUST Rukwa ni miongoni mwa Kampasi za Vyuo Vikuu zinazojengwa katika Mikoa isiyo na Taasisi za Elimu ya Juu kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), unaolenga kuboresha miundombinu, kuongeza matumizi ya teknolojia za kidijitali na kufadhili masomo kwa Wanataaluma wa Vyuo nufaika.

Ni matarajio yetu kupitia Kampasi hiyo vijana wa mkoa wa Rukwa na Mikoa mingine jirani katika ukanda wa nyanda za Juu Kusini na Magharibi watanufaika na mafunzo mbalimbali yatakayowawezesha kuimarisha ujuzi katika fani za Kihandisi na hivyo kushiriki katika maendeleo ya uchumi wao na Taifa kwa ujumla.

Tunaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ndio msimamizi mkuu katika sekta hiyo kwa kuendelea kufanya mageuzi ya elimu katika nyanja mbalimbali na kuendelea kusimamia kikamilifu uboreshaji wa miundombinu ya elimu katika ngazi mbalimbali, kuhakikisha Watanzania wanapata elimu bora.

Ni imani yetu kuwa Watanzania watatumia vema fursa kupata mafunzo katika Vyuo Vikuu na Vya kati hapa Nchini na kuwa wahitimu mahiri watakaoshiriki kikamilifu katika sekta mbalimbali za uzalishaji na kumudu ushindani katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.



## Uwekezaji Elimu ya Ufundi Stadi >




# Rais Samia aweka jiwe la msingi Chuo cha VETA Rukwa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Julai 16, 2024, ameweka jiwe la msingi chuo cha VETA kilichopo katika kijiji cha Kashai, Kata ya Momoka, wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa, ikiwa ni sehemu ya ziara yake mkoani Rukwa.

Mhe. Rais amesema kwa sasa mkoa wa Rukwa unakua kiuchumi, hasa katika eneo la miradi mbalimbali ya maendeleo, hivyo ni wakati wa vijana na jamii kwa ujumla kupata chuo cha kuwawezesha kupata ujuzi, utaalamu na maarifa ili waweze kuendana na kasi ya mabadiliko hayo makubwa ya kiuchumi.



"Chuo hiki ni jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba vijana na jamii yetu inatayarishwa na kupewa elimu ujuzi utakaowasaidia kujitegemea kwa kujiajiri au kuajiriwa," amesisitiza.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuweka msisitizo katika ujenzi wa vyuo vya VETA kote nchini na kuhakikisha kwamba kazi kubwa waliyopewa ya kuhakikisha Watanzania wanapata mafunzo ya ufundi stadi inatekelezwa kwa ufanisi.

Akitoa taarifa fupi kuhusu mradi huo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) CPA Anthony Kasore amesema ujenzi wa Chuo hicho umefikia asilimia 90% na umegharimu zaidi ya shilingi Bilioni 6, ukiwa na jumla ya majengo 24 ambayo ni pamoja na Jengo la utawala 1, Nyumba za watumishi 3, Karakana 8, Jengo 1 la madarasa (General Classes), kibanda cha mlinzi 1, Nyumba ya Jenereta 1, Jiko na bwalo la kulia chakula 1, Maktaba 1, Mabweni 4 na Maabara ya kumpyuta 1.

CPA Kasore ameongeza kuwa Chuo hicho kilianza kutoa mafunzo rasmi Machi 18, 2024 kwa Wanafunzi 63 wa fani mbili za Mafunzo ya muda mrefu za Umeme wa majumbani yenye wanafunzi 49 na Ubunifu wa nguo, ushonaji na teknolojia ya mavazi yenye wanafunzi 14.

"Pamoja na kozi hizi mbili (2) za muda mrefu tulizokwishaanza kuzitoa, tunatarajia kuongeza kozi nyingine 7 za Uashi, Uungaji na Uundaji vyuma, Ufundi Magari, Uhazili na Matumizi ya Kompyuta, Upishi, Useremala na Uchakataji wa Chakula ifikapo Januari 2025," alisisitiza CPA Kasore.

## Uwekezaji Elimu ya Juu >

# Samia aweka jiwe la msingi ujenzi wa MUST Kampasi ya RUKWA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amekitaka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kitakapokamilisha ujenzi wa Kampasi ya Rukwa kutoa mafunzo kwa vijana wa mkoa wa Rukwa ya namna ya kutumia rasilimali zinazopatikana katika mkoa huo.

Rais ametoa wito huo Julai 17, 2024 wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Kampasi hiyo, ambapo amesema kuwa Mkoa huo una rasilimali ya udongo ambayo inaweza kutumika kutengeneza matofali na kwamba ni imani yake Chuo hicho kitajielekeza kutoa mafunzo ya shughuli zinazofanywa na mkoa huo katika kukuza uchumi wao.

"Idara ya Uhandisi iwafundishe vijana wa mkoa huu kutumia rasilimali iliyopo ya udongo wajenge nyumba zinazofanana na wenzetu wa nchi zinazoendelea na zipangiliwe vizuri ili vijana wetu wapate kazi ya kufanya" aliagiza Rais Samia.

Mhe. Samia amesema kuwa ni maendeleo makubwa kwa Taifa kutekeleza ujenzi wa Kampasi hiyo mkoani Rukwa kwani miaka ya nyuma hatukuweza kufikiria kama tungekuwa na Kampasi ya chuo kikubwa kama hicho.

"Mradi wa HEET umetuletea mapinduzi makubwa sana kwenye Elimu ya Juu, kama tulivyoona tulifanya mageuzi makubwa kwenye elimu kwenda kwenye ujuzi. tunaposema elimu ujuzi tafsiri yake ni hii lazima iwe kwenye vitendo kwa kujenga Vyuo vya aina hii na Vyuo vya Ufundi Stadi ili vijana wetu wawe na Amali za mikono" alisema Mhe. Samia.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kuwa Kampasi za Vyuo Vikuu zinazojengwa katika Mikoa isiyo na Taasisi za Elimu ya Juu kupitia Mradi wa Elimu ya juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) zinatarajiwa kuanza kutoa shahada za Amali ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa mageuzi ya elimu nchini.

"Tayari nimeshafanya mazungumzo na kukubaliana na Makamu Wakuu wa Vyuo kwamba Kampasi kubwa mfano UDSM, MZUMBE na SUA ziendelee kutoa shahada za kitaalam lakini Kampasi hizi mpya zinazoendelea kujengwa zilenge katika kutoa mafunzo na Shahada za Amali" alisema Prof. Mkenda.

"Ujenzi wa Kampasi ya MUST Rukwa ni moja ya Kampasi zinazojengwa nchi nzimz kwa maelekezo yako baada ya kupata Mradi wa HEET ambapo uliagiza Mikoa isiyokua na Kampasi ya Vyuo vikuu ipate Kampasi hizo ili kutoa fursa za mafunzo kwa vijana. Alibainisha Waziri Mkenda.

Mradi huo wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Kampasi ya Rukwa unaujengwa na serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Kampasi hiyo itakuwa na uwezo wa kuhudumia Wanafunzi zaidi ya 1,000 kwa wakati mmoja.

Michezo na Elimu >



# Michezo itasaidia vijana kujiepusha na vitendo viovu

Imeelezwa kuwa, Serikali itahakikisha michezo inaendelezwa shuleni kwa sababu inasaidia vijana kujiepusha na matendo yasiyofaa.

Hayo yamesemwa Julai 20, 2024 na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda wakati wa ufunguzi wa mashindano ya mpira wa miguu ya Wazazi Dar es salaam Super Cup yaliyoanza kutimua vumbi rasmi katika viwanja vya Bandari Jijini Dar es salaam,

Mkenda ameongeza kuwa kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 michezo ni amali inayofundishwa katika shule na vyuo, vilevile inasaidia kutoa ajira na kujenga uzalendo.

Waziri Mkenda ameahidi kuendelea kushirikiana na Jumuiya za Wazazi Taifa na Mikoa.

Amepongeza Jumuiya ya Wazazi Dar es salaam kwa juhudi kubwa za kuanzisha na kuendeleza michuano.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Dar es Salaam Bi. Khadija Ally Said amesema mashindano hayo yana lengo la kukuza vipaji vya vijana pamoja na kuleta malezi chanya kwenye jamii.

Vile vile ameongeza kuwa mashindano hayo yanawaandaa vijana kuelekea kwenye Uchaguzi wa viongozi wa Serikali za mitaa pamoja na kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura.

Bi. Khadija amesema kupitia michezo hiyo vijana wanapata ajira pamoja na kuwaunganisha na kupata fursa ya kubadilishana mawazo lakini pia inawaunganisha wazazi.

Uzinduzi huu umeambatana na zoezi la kuchangia damu na jamii imepata nafasi ya kupima ugonjwa wa Seli Mundu.

Mshindi wa kwanza wa mashindano hayo atajinyakulia kitita cha shilingi milioni tano, mshindi wa pili milioni tatu na mshindi wa tatu milioni mbili.



Ushirikiano katika Elimu >

# Wizara ya Elimu kushirikiana na taasisi ya Vignan's ya India eneo la Sayansi, Teknolojia na Utafiti





Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetia saini makubaliano ya ushirikiano na Taasisi ya Utafiti, Sayansi na Teknolojia ya Vignan's kutoka India.

Makubaliano hayo ni katika masuala ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Utafiti ikiwa ni pamoja na taasisi hiyo kupokea wanafunzi 100 kutoka Tanzania kila mwaka kwa ajili ya kusoma fani za kipaumbele ikiwemo Uhandisi ujenzi, Uhandisi Kilimo, Akili Mnemba na Uhandisi wa Umeme kwa gharama nafuu.

Kamishina wa Elimu Dkt. Lyabwene Mutahabwa akimwalisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema bila Utafiti, Sayansi na Teknolojia ni vigumu kushindana popote.

Ameishukuru Serikali ya India na Taasisi ya Vignan's kwa utayari wa kushirikiana na Tanzania.

"Ukiwa na rafiki ambaye yupo tayari kukusaidia kwenye eneo la Elimu kwenye nchi huyo ndiye rafiki wa kweli" amesema Lyabwene.

Kwa upande wake Afisa Mtendaji wa Chuo cha Vignan's Srikant Nandigam amesema vijana wa Kitanzania watapata ujuzi na baada ya masomo watakuwa tayari kuajiriwa na kujiajiri pia hawatakaa India bali watarudi Tanzania kueneza ujuzi huo.

Amesema Taasisi ya Vignan's ina miaka 23 toka ianzishwe na kufanya kazi, huku ikiwa tayari imefanya kazi na mataifa 9 kutoka Afrika na Tanzania inakwenda kunufaika kwa mara ya Kwanza.

Tanzania ni Taifa la pili kwa kupeleka wanafunzi wengi zaidi nchini India baada ya Zimbabwe.

Mafunzo VETA >



# VETA Njombe kuanza kutoa mafunzo

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) imeagizwa kuhakikisha Chuo cha VETA cha Mkoa wa Njombe kinapelekewa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kianze kutoa mafunzo kwa wakazi wa mkoa huo.

Agizo hilo limetolewa Julai 19, 2024 na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula alipofika chuoni hapo kukagua utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ambapo alisema ameridhishwa na ukamilishaji wa majengo hayo.

Dkt. Rwezimula ameongeza kuwa majengo yote yakikamilika ni muhimu chuo kuanza kutoa mafunzo kwa wananchi wa Njombe na kwamba si sahihi yakakaa muda mrefu bila kutumika.

Aidha, amewataka vijana na wananchi wa mkoa huo kuchangamkia fursa za masomo na mafunzo yatakayotolewa katika chuo hicho huku akiwataka VETA kuhakikisha kuanzisha programu zinazoendana na shughuli za kiuchumi za mkoa huo.

Chuo cha VETA cha Mkoa wa Njombe kimejengwa katika wilaya ya Ludewa karibu sana na Mchuchuma na Liganga ambapo yanapatikana makaa ya mawe pamoja na chuma.



Uzinduzi zana za Kilimo >

# Kipanga azindua zana za kilimo zinazotengenezwa na wazawa IMARA Tech






Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omar Juma Kipanga (Mb) amesema vijana wa Kitanzania wana nguvu kubwa ya kuchochea maendeleo katika Taifa hivyo Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia makampuni mengi zaidi kuwekeza katika Teknolojia mbalimbali ambazo zinazalishwa nchini na kukidhi vigezo vya kuingia sokoni.

Kipanga ametoa kauli hiyo Julai 01,2024 wakati akizindua zana bora za kilimo zilizotengenezwa na Kampuni ya wazawa ya IMARA TECH, katika viwanja vya Makumbusho Kaloleni jijini Arusha.

“Leo tumeshuhudia mfano mzuri wa tukio kubwa la utiaji saini wa mashirikiano kati ya Imara Tech na Taasisi kubwa mbili Honda na Mfuko wa dhamana kwa wakulima-PASS wakati wa uzinduzi wa zana bora za kilimo zinazozalishwa na kampuni hiyo” alisema Kipanga.

Ameongeza kuwa hadi sasa zaidi ya teknolojia 30, zilizozalishwa na wabunifu wa ndani waliowezeshwa na Serikali kupitia jukwaa la MAKISATU na kupata ufadhili kupitia COSTECH zimefikia hatua ya kuingia sokoni.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) Dkt. Amos Nungu amesema Tangu kuanza kwa MAKISATU, zaidi ya Wabunifu 268 wameendelezwa kwa hatua mbalimbali, Kampuni 23 za vijana wa kitanzania zimesajiliwa tayari na zinatazamiwa kujenga viwanda na kuongeza uwepo wa bidhaa zao sokoni na zingine 47 ziko kwenye hatua za mwisho kukamilisha viwango na matakwa ya usajili wa Kampuni.

Aidha Mkurugenzi Mtendaji wa IMARA Tech Bw. Alfred Chengula ameishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia COSTECH na wadau wengine kwa kuendeleza bunifu hadi kufikia kubidhaishwa.

Ziara ya Kimafunzo>



# Prof. Nombo aongoza ziara ya mafunzo Afrika Kusini - ugharamiaji mafunzo ya amali



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema Tanzania imefanya mageuzi katika mitaala ambayo ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye alihimiza kufanya mabadiliko na kuwa na mitaala inayojikita katika ujuzi.

Prof. Nombo amesema hayo Julai 17, 2024 wakati akizungumza na Uongozi wa Chuo cha Ufundi cha Tshwane South nchini Afrika Kusini, kufuatia ziara yake na Wataalamu wa elimu kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kujifunza jinsi Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET) inavyogharamiwa.

Aidha, Katibu Mkuu huyo ameeleza kuwa Tanzania iko katika hatua ya kuandaa mkakati wa Ugharamiaji wa Uendelezaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET Financing Strategy) na ziara hiyo ni katika kuendelea kujifunza mifumo mbalimbali ya nchi juu ya utekelezaji wa mafunzo ya ufundi.

Prof. Nombo ameeleza kuwa ziara hii imekuwa na manufaa makubwa, ambayo yatasaidia kujifunza jinsi Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET) inavyogharamiwa.

Katika ziara hiyo chuoni hapo Katibu Mkuu ameambatana na Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi, Mkurugenzi wa Elimu Msingi na Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam.

Ikumbukwe kuwa Afrika Kusini ina jumla ya vyuo vya TVET 50 na kampasi 280 huku uelekeo wa mafunzo ya ufundi nchini humo ni vigezo vya Utengenezaji na Uboreshaji wa Mitaala. (Occupational Standards).

Mafunzo Nishati Jadidifu >



# Wataalamu wa Nishati Jadidifu kupikwa ATC kampasi ya Kikuletwa

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeweka Jiwe la Msingi la ujenzi wa Chuo Ufundi cha Arusha Kampasi ya Kikuletwa iliyopo wilayani Hai Mkoani Kilimanjaro kitakachokuwa Kituo cha Umahiri katika kutoa Nishati Jadidifu.

Akizungumza Julai 30, 2024 baada ya kuweka Jiwe hilo la Msingi Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kuwa Kituo cha Kikuletwa ni miongoni mwa vituo vinne vya umahiri vya kikanda vinavyojengwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia.

Waziri Mkenda amesema kuwa Vituo hivyo vinajengwa kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 75 sawa na takribani shilingi Bilioni 187.5 kupitia mradi ujulikanao kama East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP) ambapo Chuo cha Ufundi Arusha kilipatiwa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 16.25 sawa na takribani Bilioni 37.5

Prof. Mkenda ameongeza kuwa Ujenzi wa Kituo hicho ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/2026) na kwamba ni muhimu kwani kitazalisha nguvukazi yenye ujuzi wa kutosha itakayosaidia uendeshaji wa miradi ya kimkakati ya Kitaifa hususan katika uzalishaji wa nishati kama vile ujenzi wa Mitambo ya Kuzalisha Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere.

"Mwelekeo wa Dunia sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunatumia nishati safi na endelevu bila kuharibu mazingira, hivyo kituo ni muhimu sana na kinaendana na azma ya Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba tuwe na nishati safi ya kupikia na matumizi mengine ni hatua kubwa katika mwelekeo wa Dunia ya kulinda mabadiliko ya tabia nchi kwa kuhakikisha kwamba hatuchomi mafuta kama dizeli yanayokwenda kuharibu hali ya hewa" amesema Prof Mkenda

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema kuwa Mradi wa Kujenga na Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki (EASTRIP) ni muhimu kwa kuwa una kwenda kusaidia katika utekelezaji wa mabadiliko ya kielimu ambayo yameanza kutekelezwa kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, Toleo la 2023 pamoja na Mitaala mipya katika ngazi mbalimbali.

Prof. Nombo amesema kuwa Tanzania ina vituo vinne vya Umahiri ambavyo ni Kituo cha Umahiri cha Kikanda katika Mafunzo ya Nishati Jadidifu katika Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kinaanzisha kituo cha umahiri cha Kikanda katika mafunzo ya Usafirishaji wa Anga na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ambacho kina Vituo viwili vya Umahiri ambavyo ni Kituo cha Umahiri cha Kikanda katika Tehama kupitia Kampasi ya Dar es Salaam na kituo cha Umahiri cha Kikanda katika Teknolojia ya Ngozi katika Kampsi ya Mwanza.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mkuu wa Wilaya ya Hai Mhe. Amiri Mkalipa ameishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kujenga Kampasi hiyo ambayo itainua Uchumi wa wana Hai na Kijiji cha Cheemka kwa kuwa kuna uzalishaji wa mazao ya vyakula ambayo yatatumika katika kulisha wanachuo wa kampasi hiyo.



Marufuku kufukuza Mwanafunzi >

# Marufuku kufukuza mwanafunzi kwa kushindwa kuchangia mchango wowote - Waziri Prof. Mkenda









Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema ni marufuku Mwanafunzi yeyote kufukuzwa kwenye shule za umma, kurudishwa nyumbani kwa sababu mzazi ameshindwa kuchangia mchango wowote ikiwemo huduma za chakula.

Mkenda ametoa agizo hilo Julai 26, 2024 jijini Dodoma wakati akizungumza katika Kongamano la Utoaji Chakula na Lishe Shuleni, akisisitiza mzazi anayekataa kuchangia mchango uliowekwa kulingana na miongozo waliyojiwekea Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kuchukua hatua dhidi ya mzazi wakati Mwanafunzi akiendelea na masomo.

Akihutubia Kongamano hilo Waziri huyo amewataka Wadau mbalimbali kuendelea kushirikiana kuhamasisha huduma ya chakula kwa Wanafunzi wakiwa shuleni.

"Lishe bora shuleni ni msingi muhimu katika maendeleo ya kiafya na kiakili na kwamba inachangia Mwanafunzi kujifunzaji kwa ufanisi. Mwanafunzi anapokosa chakula hukabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo njaa, utoro wa rejareja na hata kukatisha masomo kwa baadhi yao" alisema Mkenda.

Katibu Mkuu wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema bado kuna uhitaji mkubwa wa kuhamasisha jamii na wadau mbalimbali kushiriki kikamilifu katika kuhamasisha na kuchangia uwepo wa huduma hii katika shule za Awali, Msingi na Sekondari.

Amesema Kongamano hilo, limewakutanisha Wataalam kutoka Wizara za kisekta Mashirika mbalimbali na Vyuo Vikuu ambao wamejadili mada mbalimbali ikiwa ni pamoja na Uendelezaji wa Programu ya chakula shuleni, Huduma za afya na lishe shuleni pamoja matumizi ya vyakula vilivyorutubishwa na Upatikanaji wa taarifa za utoaji wa huduma ya chakula shuleni.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule ameipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia na kufuatilia suala la lishe Shuleni, hali inayochochea afya na elimu bora katika mkoa huo.

Amesema katika kipindi cha mwezi Januari hadi Machi 2024, Shule za Msingi za Serikali 854 zenye Wanafunzi 437,749 sawa na asilimia 70 ya Wanafunzi zimeweza kutoa huduma ya chakula na Sule za Sekondari 261 zimetoa chakula kwa Wanafunzi 143,700 sawa na asilimia 69.2

Akitoa neno Mwakilishi wa Balozi wa Marekani Nchini Bw. Paul Alberghine ameipongeza Serikali kwa kutilia mkazo suala la chakula na lishe Shuleni, pamoja na mashirikiano mazuri kupitia Mpango wa Kimataifa wa McGovern-Dole wa Chakula kwa Elimu na Lishe ya Watoto tangu 2010.

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

---

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

---

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

---

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

---

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

---

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

---

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

---

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

---

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz